# MAELEZO KUHUSU TaTEDO - SESO

**TaTEDO-Sustainable Energy Services Organization** (TaTEDO-SESO) ni taasisi isiyo ya kiserikali inayotoa na kuendeleza huduma za nishati endelevu nchini Tanzania. Taasisi hii ilianzishwa mwaka 1990, zaidi ya miaka 30 iliyopita. Makao makuu yake yapo Dar es Salaam, Tanzania na pia ina ofisi ndogo katika jiji la Dodoma na Moshi mjini na inafanya kazi kupitia wadau wengine ndani na nje ya nchi.

## Maono

Watu wote ndani ya nchi waweze kupata huduma za nishati endelevu, wakiendelea kuhifadhi mazingira, kutengeneza kipato na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

## Dhamira

Kuwezesha na kufanikisha wadau kujenga uwezo kwa kuondoa changamoto kwenye mnyororo wa thamani wa nishati endelevu, kutoa huduma saidizi na mazingira wezeshi ya kupata nishati endelevu huku tukihifadhi mazingira, kuongeza kipato na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

## Malengo

* Kuboresha ubora wa Maisha ya Watanzania kwa kuchangia uwepo na upatikanaji wa nishati endelevu, ajira na fursa za kuongeza kipato, vyote vikiwa muhimu katika kupunguza umaskini.
* Kupunguza uharibifu wa mazingira utakanao na kuongezeka kwa matumizi ya kuni, mkaa na mafuta.
* Kusaidia Nchi kupunguza utegemezi wa nishati za kuagizia kutoka nje ya nchi.

## Madhumuni

Madhumuni ya TaTEDO-SESO ni kuboresha maisha ya watu kwa kuongeza upatikanaji wa huduma na matumizi ya nishati endelevu.



*Mtambo na mtandao mdogo wa kuzalisha na kusambaza umeme maeneo ya vijijini.*

## Kazi Kuu

**TaTEDO-SESO** hushirikiana na wadau mbali mbali ili kufanikisha upatikanaji wa nishati endelevu nchini Tanzania kwa kuendeleza utaalamu wa kuongeza upatikanaji na matumizi ya nishati endelevu kwa kutekeleza yafuatayo:-

* Kuendeleza na kutekeleza kwa njia shirikikishi kwenye kuchambua, kupanga na kutekeleza kazi vijijini na mijini.
* Kuendeleza na kusaidia teknolojia na huduma za nishati endelevu kwenye mnyororo wa thamani kwa kutafuta vyanzo, wadau, changamoto na hatimaye kusanifu na kufanikisha upatikanaji wa nishati endelevu kwenye ngazi tofauti za kijamii.
* Kuendeleza na kutekeleza huduma saidizi (kama uhamasishaji, kujenga uwezo wa ufundi na biashara na kuunganisha wateja na wajasiriamali na vyanzo vya fedha ili kuwapa uwezo wa kununua na kuendeleza biashara.
* Kukuza mazingira wezeshi (kwa kuwasiliana, kukutana na kujadiliana na watunga sera na wafanya maamuzi kitaifa na kimataifa ili waweze kuandaa na kutekeleza sera, mikakati, na sheria wezeshi ili kutoa motisha wa kuongeza maendeleo na matumizi ya nishati endelevu.



*Spika wa Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania akipokea Jiko la Umeme Lenye Presha kutoka kwa Afisa Mtendaji Mkuu wa TaTEDO-SESO, Dodoma, Tanzania*

## Mafanikio

Katika kuendeleza na kukuza huduma, teknolojia na masoko ya nishati endelevu, **TaTEDO-SESO** inalenga kukuza aina mbili za nishati; nishati za tungamoto taka na za umeme. Katika kukuza nishati za tungamotaka, juhudi zipo kwenye upatikanaji na matumizi ya majiko sanifu, uzalishaji mkaa kwa njia endelevu ukiwemo mkaa mbadala. Taasisi imeweza kusambaza zaidi ya majiko milioni mbili (2) ambayo yanaambatana na utoaji wa mafunzo kwa mafundi na wataalam 1,500.

Juhudi za kuendeleza matumizi sanifu ya nishati ya umeme zimejitokeza zaidi kwenye kuhamasisha maendeleo na matumizi ya umeme utokanao na mionzi ya jua kwenye kaya na taasisi za huduma za kijamii, kama hospitali na mashule. TaTEDO-SESO pia imehamasisha na kukuza mitandao ya umeme mdogo yenye uwezo usiozidi 100Kw. Zaidi ya mitambo 21 iliendelezwa na utafiti kuhusu uendelevu, ushirikishwaji na usimamizi wake ulifanyika na ripoti kadhaa ziliandikwa na kusambazwa.

Uhamasishaji wa matumizi ya umeme kupikia kwa kutumia majiko sanifu ya umeme yenye presha umefanyika na zaidi ya kaya 13,000 sasa hivi zinatumia aina hiyo ya majiko. Juhudi za kuendeleza na kuhamasisha matumizi ya umeme kuendesha vyombo vya usafiri zimeanza na mategemeo ni kuweza kupata mafanikio zaidi kwenye eneo hili.



*Maonyesho ya Jiko la Kuni la Taasisi Lenye Ufanisi wa Juu katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Masasi, Wilaya ya Masasi, Mkoa wa Mtwara*




*Mafunzo kuhusu tanuri sanifu la kuchomea mkaa*

## Teknolojia za Nishati Endelevu

Zifuatazo ni teknolojia za nishati endelevu zinazokuzwa na TaTEDO-SESO:-

* Mitambo na mitandao midogo ya umeme utokanao na nishati endelevu.
* Majiko tofauti sanifu ya nishati za kuni na mkaa.
* Mifumo na teknolojia za uzalishaji umeme utokanao na mionzi ya jua.
* Makaushio ya Jua, madogo na makubwa ya kibiashara.
* Uzalishaji mkaa kwa njia na teknolojia endelevu.
* Uzalishaji mkaa mbadala toka mabaki ya mimea na mazao.
* Majiko tofauti sanifu ya umeme.
* Vyombo vya usafiri vitumiavyo umeme.mfano kile cha magurudumu matatu.



*Ukaushaji wa Mazao kwa Kutumia Nishati ya Jua*

## Njia za Utekelezaji

TaTEDO-SESO uhutekeleza kazi zake kwa njia ya ushirikishwaji, ili kuendeleza wadau, huduma na teknolojia katika mnyororo wa thamani wa nishati endelevu. Hii ni pamoja na kufanya yafuatayo:

| Mnyororo wa thamani wa nishati endelevu | Huduma saidizi | Mazingira wezeshi |
|---|---|---|
| Uchambuzi na Utambuzi wa Wadau katika Mnyororo wa Thamani wa Nishati Endelevu. | Kutambua na kuhakikisha upatikanaji wa huduma saidizi kama vile uhamasishaji, upatikanaji wa mitaji na msaada wa kifedha. | Kufanikisha uwepo wa mazingira wezeshi kutokana na kupatikana kwa sera saidizi, mitaji, fedha, mikakati na sheria. |
| Kuainisha changamoto za kila mdau. | | |
| Kuchambua na kuelewa vipaumbele vya wadau na jinsi vinavyohusiana na huduma za nishati endelevu. | Kujenga uwezo kwa njia ya maonesho na mafunzo. | |
| Kuchambua masuala ya kijamii, uchumi na kitamaduni ya watumiaji wa nishati endelevu kama vile kiwango cha ufahamu uwezo na nia ya kulipia huduma za nishati endelevu. | Kusimamia na kusambaza taarifa za kuhamasisha. | Motisha kwa ajili ya kuwezesha kupatikana mazingira wezeshi kama vile ruzuku, misamaha ya kodi na ushuru nafuu. |
| Kupanga na kutekeleza na wadau kazi na hatua sahihi za kuendeleza nishati endelevu kama ubunifu, mitandao ya wadau, vikundi vya kijamii, nk. | Kukutanisha watumiaji na wajasiriamali na huduma za kifedha kwa ajili ya mitaji ya uwekezaji na kuendeshea biashara. | |



*Maonyesho ya Vifaa vya Kupikia kwa Umeme katika Kijiji*

TaTEDO-SESO, Mbezi Juu, Nyumba Namba 28, Barabara ya TaTEDO, karibu na KKKT Mbezi Juu, Goba, Ubungo, S. L. P. 32794, Dar es Salaam, Tanzania. Simu: +255-738-201498, BaruaPepe: energy@tatedo.or.tz, Tovuti:www.tatedo.or.tz
Ofisi ya Dodoma: +255-736-700771.Ofisi ya Moshi: +255-767-000722)

TaTEDO-SESO inatoa shukrani za dhati kwa Serikali, Washirika wa Maendeleo na wadau wengine kwa msaada na michango yao kwa ajili ya kufanikisha juhudi zetu.

TaTEDO-SUSTAINABLE ENERGY SERVICES ORGANIZATION

TaTEDO-SESO

Nishati Safi kwa Wote

**Taasisi ya Huduma za Nishati Endelevu ya TaTEDO**

# TaTEDO-SESO KWA UFUPI




*Sisi Wazee Hili Jiko Limetusaidia Sana Kupika Vyakula Dawa*

## Imejitoa Kufanikisha Upatikanaji na Kuwezesha Utumiaji wa Huduma za Nishati Endelevu kwa Watu wote